



SHULE YA UPILI YA MANGU

JINA: _____

NAMBARI: _____ SAHIHI: _____

TAREHE: _____

102/2
KISWAHILI
Karatasi ya 2
(LUGHA)
MTIHANI WA MWIGO
JULAI 2016
MUDA: Saa 2½

SHULE YA UPILI YA MANGU
MTIHANI WA MWIGO
Kiswahili
Lugha
Karatasi 2
Muda: saa 2 ½

MAAGIZO

- Andika jina lako na nambari yako katika nafasi zilizoachwa hapo juu
- Tia sahihi yako kisha uandike tarehe
- Karatasi hii ina maswali manne (*Ufahamu, Ufupisho, Lugha na Isimujamii*)
- Jibu maswali yote kwenye nafasi zilizoachwa baada ya kila swali

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

| | Swali | Upeo | Alama |
|---|-------------------|-------------|--------------|
| 1 | Ufahamu | 15 | |
| 2 | Ufupisho | 15 | |
| 3 | Matumizi Ya Lugha | 40 | |
| 4 | Isimujamii | 10 | |
| | JUMLA | 80 | |

Fungua ukurasa

1. UFAHAMU

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Bwana Gimbi alikuwa mlevi wa kutajika kijijini mwake. Hakuna aliyekosa kusimulia kisa cha Mzee huyu. Gimbi hakusifiwa tu na wapiga maji wenzake kwa umahiri wake katika kuubugia uji mchachu, bali pia alisifiwa na watoto wa vijana na kijijini kwa sauti yake ya ninga, hasa alipokuwa ameonja zake mbili tatu.

Gimbi alikuwa mfanyikazi katika shamba moja ya mkwasi aliyepanda chai kwa madhumuni ya kuiuza ughaibuni. Mshahara wa Gimbi haukuwa wala haukuwa mdogo mno, kwani ndiye aliyekuwa msimamizi wa shamba hili. Kipato alichopata kingeweza kuikidhi familia yake ya watoto na mke mmoja ambaye pia alifanya kazi katika shamba la mkwasi yuyu huyu. Hata hivyo, Bwana Gimbi alikuwa daima yu waya. Kila mwisho wa mwezi ulimwengu mzima ulimtambua. Alikuwa na hulka ya kuamka alfajiri na mapema Ijumaa ya mwisho wa mwezi kuelekea posta kuutwaa mshahara wake. Mara tu baada ya kuupokea mshahara wake, Gimbi angeshika njia hadi kwa mgema mashuhuri mtaa wao na kupiga kachombe kwenye vidimbwi vya pombe hadi misuli ya tumbo lake ilipochoka na kulalamika. Baada ya kuogelea ko huku, Gimbi angekuwa hana hanani, na kuarudia masikini mkewe, uso kauinamisha kwa tahayuri.

Nyumbani mkewe, mama Mtima, angepata kibarua kingine cha kumungaza simba wake kwa siku kadha kabla yeye Gimbi hajarudi kazini. Ilimbidi Mtima kuyatibu maradhi ya Gimbi ambayo hayakusikia dawa nyingine ila mchuzi wa nyama. Mtima alijibidiisha kwa vyovyote vile kumtibu mumewe huyu, hasa siku za mwanzo mwanzo. Baadaye stahama ilianza kumwishia hasa baada ya kugundua kuwa mzigo wa malezi ya wanawe ulimlelea yeye. Alianza kumsihi mumewe aache mchezo huo ambao ulimushia kumfanya amwage unga wake kudhoofisha zaidi afya yake ambayo tayari ilikuwa inadidimia. Hata hivyo, maneno ya Mtima yaliangukia moyo wa jabali lisilosikia la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Gimbi alikata katakata kuacha uraibu wake huu huku akidai kuwa mume asiyeonja vileo hayamudu maendeleo, na kwamba hawezi kukubali kudhibitiwa na mwanamke asilani.

Mtima alizungumza na mumewe, hadi alipokata tamaa na kukata kauli kumwenda mshauri mmoja aliyekuwa na kliniki yake hapo mtaani kulilia hali yake. Mshauri huyu alipozungumza na bwana Gimbi, Gimbi alijawa na hamaki kubwa. Akalalamika kwamba mkewe alikuwa amemvua nguo hadharani na kuapa

kumpatiliza. Jioni hiyo nyumbani mwa Gimbi kulisikika kilio kikubwa zaidi ya kile cha kawaida. Majirani, ambao walikuwa wameizoea tabia hii ya Gimbi kumpiga mkewe mara kwa mara, walikuwa wameamua kutoyaingilia masuala yasiyowahusu. Hata hivyo vilio vya watoto viliwatia imani, wakaamua kumkabili hasidi huyu. Gimbi alipoombwa kufungua mlango wa nyumba alikataa, akidai kwamba haikufaa majirani kuingilia mambo yake ya unyumba. Hata hivyo baada ya shinikizo la majirani, alifungua, akatoka na kujiendea zake kumwacha Mtima kuwamwagia kuku mtama.

Mtima aliwaeleza majirani masaibu aliyokuwa ameyapata. Alisema kwamba bwana Gimbi ametelekeza familia yake. Hakujua njaa wala shibe ya watoto wake. Karo ya watoto alilipa yeye Mtima na aliposhindwa kulipa, watoto walifukuzwa shule, ulevi wa Gimbi ulikuwa umemtia kwenye madeni ambayo yeye mara kwa mara yeye Mtima alilazimika kuyalipa kuepuka fedheha ya wadi ya mumewe. Sasa alikuwa amefikia ukingoni, ikabidi amwendee mshauri, ndipo akapata jaza ya kipigo.

Baada kusikiza kisa cha Mtima, mmoja wa majirani alimshauri Mtima kumwendea mwajiri wa Gimbi na kushitakia hali. Aliandamana na Mtima hadi kwa tajiri wa Gimbi. Tajiri huyu alisikitika sana na kukashifu kutowajibika kwa Gimbi. Alimwita Gimbi mbele ya mkewe na jirani yake na kumwambia kuwa ingebidi, aidha akubali robo tatu mshahara wake uwaendee wanaye hadi pale atakapobadilika au ajiuzulu kazi. Gimbi hakuwa na budi. Alikubali shingo upande kumpa mkewe robo tatu za mshahara wake kila mwezi ili kukidhia mahitaji ya familia yake. Robo iliyobaki Gimbi alitwaa yeye kwa mahitaji yake ya kibinafsi. Baada ya kisa hiki cha kufedhehesha, Gimbi aliapa kuacha ulevi. Alimtupa jongoo na mti wake; akaacha kuandamana na marafiki waliomhimiza kulewa kila mara. Hali ya familia yake ikaimarika, watoto wakaacha kufukuzwa shule, naye Gimbi siha yake ikaanza kunawiri.

Maswali

- (a) Ni mambo gani yaliyomfanya Gimbi kusifiwa katika mtaa wake? (al. 2)
- (b) Kulingana na taarifa, ulevi huathiri vipi jamii? (al. 4)

(c) Mtima alifanya nini kumsaidia mumewe kuacha ulevi? (al. 3)

(d) Majirani na mwajiri wake wamezingatia haki za kibinadamu vipi? (al. 2)

(e) Eleza maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa kwenye kifungu (al. 4)

(i) Kudhibitiwa

(ii) Kutupa jongoo na mti wake

(iii) Masaibu

(iv) Kufedhehesha

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu mawali yanayofuata.

Sanaa ya jadi ni njia moja ya mawasiliano ambayo ni adhimu, hasa barani Afrika. Mawasiliano kupitia kwa sanaa ya jadi ni njia bunifu ya kuwasilisha ujumbe kupitia kwa sanaa tendi kama vile drama, ushairi tendi, masimulizi nyimbo, ngoma na kadhalika. Njia hii imekuwa ikitumika katika jamii nyingi za Kiafrika toka jadi kwa ufanisi mkubwa sana, kuwasilisha ujumbe kwa wanajamii, hasa hekima na busara ya wakongwe kwao chipukizi.

Takribani katika jamii zote za Kiafrika, sherehe yoyote ya jadi haikukosa sanaa tendi. Lazima pangekuweko na sanaa tendi katika sherehe kama vile tohara, kutakaswa na kutawazwa kwa viongozi, mazishi, ndoa na hafla za burudani. Licha ya kuburudihisa na kuchangamsha waliohudhuria, sanaa hizi zilitumika kuwasilisha na kupasha ujumbe. Sanaa hizi hata hivyo hazijapitwa na wakati na bado zinaweza zikatumika sambamba na njia za kisasa na mawasiliano kama vile redio, runinga, magazeti, majarida na wavuti.

Matumizi ya sanaa ya jadi pamoja na njia za kisasa za mawasiliano yana manufaa lukuki. Kwanza, matumizi haya yataweza kuwashirikisha kikamilifu watu wengi katika mawasiliano, hasa akika yahe wa mashambani na wanaotoka katika mitaa ya mabanda ambao huhisi wametengwa na njia za kisasa za mawasiliano. Aghalabu, njia za kisasa za mawasiliano huchukuliwa na baadhi ya wanajamii kuwa ni milki ya walioelimika, walio mijini na hasa wenye ushawishi mkubwa katika kuunda na kutekeleza sera zinazotawala nchi.

Hali kadhalika, mawasiliano huchukuliwa kuwa ni himaya ya watu wanaojiweka mbele kuwa wajuzi wa kila kitu. Wao huzitumia njia hizo kuendeleza maslahi yao kwa kutoa maamuzi yanayowaathiri hata waliotengwa, bila kuwashirikisha katika maamuzi hayo. Fauka ya haya, njia za kisasa za mawasiliano hutumia lugha ambazo hazifahamiki na wengi. Aghalabu hutumia lugha za kigeni kama vile Kingereza na Kifaransa, ati kwa kuwa ndizo lugha za kimataifa na lugha tukufu, ingawa ujumbe unaowasilishwa na lugha hizo huusiwa kwa namna yenye utata na isiyoeleweka na wengi. Matokeo ya ujumbe huo ni athari kwao pamoja na vizazi vyao. Isitioshe, njia hizi huwa ghali na pia huchukuana na teknolojia inayokanganya. Hali hizi ndizo huchangia kutngwa kwa wanajamii na viongozi, na kuwafanya watumiaji baridi wa njia hizi za mawasiliano kwa kuwakosesha fursa ya kutoa mwitiko ama michango yao kupitia kwa njia hizi.

Kwa upande mwingine, matumizi ya njia ya sanaa za jada hushirikisha watu wote – walioelimika na wasioelimika. Hii ni kwa kuwa njia hii haitegemei matini yaliyoandikwa. Pili, njia hii haitumii teknolojia inayokanganya na iliyo ghali. Zaidi ya haya, njia ya sanaa za jadi hupasha ujumbe huku ikichangamsha, kuburudisha, kuteka na kuwavutia wengi huku ikidumisha urazini na taharuki zao. Aidha, sanaa za jadi hutoa nafasi ya kurudia igizo au onyesho na kuwasilisha jumbe anuai kwa muda mfupi sana.

Sanaa ya jadi, kama njia ya mawasiliano, hutoa nafasi sawa kwa watu wote kuelimika na kupata maarifa bila kubagua kwa misingi ya umri au jinsia. Hii ni kwa kuwa wakubwa kwa wadogo, chipukizi kwa wakongwe, wake kwa waume na wavulana kwa wasichana wanaweza wakashiriki katika maonyesho au maigizo. Sanaa tendi za kifaraka aidha hutoa nafasi kwa hadhira kushiriki. Njia hii pia ni maarufu katika kuzindua, kuhamasisha, na kusambaza ujumbe kwa watu wengi bila kuwachosha wala kuwasinya. Licha ya kuwa ina uwezo wa kumchongoa na kumchambua mtu kwa wakati huo huo, ina uwezo pia wa kumfanya mtu asijihisi kuwa anaingiliwa, kusimangwa, kukashifiwa wala kufanyiwa stihizai. Hivyo basi, hakuna kwenda mahakamani kushtaki na kudai fidia kama ilivyo katika njia za mawasiliano za kisasa. Sanaa tendi huwa hailengi mtu mahususi bali kaumu inayoshiriki, na kila mmoja huathirika kivyake.

Maswali

- (a) Kwa maneno kati ya 40-50, eleza mambo yote muhimu anayozungumzia mwandishi katika aya ya kwanza na ya pili. (al. 6 na 1 ya mtiritiko)

Nakala chafu

Nakala safi

- b) Fupisha ujube katika aya ya tatu, mne na tano kwa maneno kati ya 100-110.
(alama 7 na alama 1 mtiririko)

Nakala chafu

Nakala safi

3. MATUMIZI YA LUGHA (AL. 40)

- a) Taja sauti zenye sifa zifuatazo
i) Kizuiwa hafifu cha kaakaa laini (al.2)
- ii) Kikwaruzo ghuna chan ufizi
- b) Fafanua majukumu mawili ya shadda (al.2)
(i)
(ii)
- c) Tunga sentensi moja moja kulingana na maagizo (al.2)
i) Sentensi yenye kiwakilishi kinachotumika badala ya nomino ambayo habari zake zinasisitizwa
ii) Sentensi yenye kielezi cha namna kinachoonyesha mbinu ya kufanikisha kitendo.
- d) Taja vigezo viwili vya kuainisha viambishi (al.2)
- e) Fafanua aina mbili za mazizi na utolee kila aina mfano (al.2)
- f) Eleza miundo miwili ya nimino katika ngeli ya LI-YA (al.2)
- g) Bainisha nyakati mbili zinazowakilishwa na kiambishi kilichopigiwa mstari (al.2)
Sisi twapenda kula maharagwe
- h) Andika kinyume
Furaha aliketi karibu na msichana aliyeombwa kukusanya vitabu
- i) Andika katika usemi halisi (al.2)
Kibwana alishangaa kuwa huyo alienda bila kumuaga
- j) Tunga sentensi kudhihirisha makundi mawili ya nomino ambapo neno hili laweza